N03/251/S(1)T

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Tuesday 4 November 2003 (morning)
Mardi 4 novembre 2003 (matin)
Martes 4 de noviembre de 2003 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1 (Text handling).
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir ce livret avant d'y être autorisé.
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1 (Lecture interactive).
- Répondre à toutes les questions dans le livret de questions et réponses.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos requeridos para la Prueba 1 (Manejo y comprensión de textos).
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# Viashirio (Dalili)

- Viashirio vya ushirikishwaji:
  - Idadi ya washiriki na ushiriki katika warsha za mashauriano
  - Ushiriki wa makundi ya jumuiya
  - Usambazaji wa ripoti za serikali
- Ripoti za kila miezi minne kuhusu maendeleo ya mageuzi ya mfumo wa mahakama na uchunguzi wa rushwa.



**KIFUNGU B**

# Samaki na dagaa wapungua Ziwa Tanganyika

***NA NSWIMA EARNEST, MBEYA***

**UVUVI na samaki na dagaa katika Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa umepungua kutokana na sababu za ukame, uharibifu wa mazingira na hali ya wasiwasi wa usalama na hivyo kusababisha kupanda kwa bei ya bidhaa hizo.**

Uchunguzi uliofanywa na *HEKO* kwenye soko kuu la mjini Sumbawanga umegundua kuwa kilo moja ya dagaa kutoka Ziwa Tanganyika imepanda kutoka shilingi 800 hadi shilingi 1,800 na samaki wabichi kutoka shilingi 300 hadi shilingi 900 kwa kilo.

Mmoja wa wachuuzi maarufu wa bidhaa hizo katika soko hilo Spensa Chenjelu alisema licha ya hali mbaya ya hewa kwenye maziwa hayo hali ya usalama wa maisha ya wavuvi inachangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa kasi za shughuli za uvuvi.

Alisema wavuvi wa ziwa Tanganyika huhofia usalama wa kuvua katika Ziwa kwenye mkondo mkubwa wa dagaa kwa kuhofia kuporwa zane zao za uvuvi na maharamia wanaosadikiwa kutoka nchi za jirani.

Kutokana na ukweii huo alisema inabidi wavuvi wafanye shughuli zao kando kando ya Ziwa kwenye uchache wa dagaa na samaki na kupunguza kiwango cha uvuvi.

Afisa uvuvi wa mkoa wa Rukwa Emmanuel Katembo alikaririwa na *HEKO* akisema kuwa moja ya tatizo linalopelekea kuadimika kwa samaki na hasa katika Ziwa Rukwa ni uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ongezeko kubwa la mifugo na kilimo kisichokuwa na utaratibu.

Katembo alisema Ziwa Rukwa limekuwa likijaa matope (SILTATION) na kwamba wavuvi hushindwa kuvua kutokana na matope hayo na alisema ipo hatari kwa Ziwa hilo kuendelea kupungua kina chake mwaka hadi mwake. Afisa huyo wa mkoa wa Rukwa ametoa wito kwa wananchi mkoani humo kuendelea kuboresha na kutunza mazingira ambayo alisema ni chanzo kikubwa cha upatikanaji wa mahitaji yote muhimu kwa binadamu viumbe wengine.

**KIFUNGU C**

# MOTO

I Hapo kale watu walikuwa wanakula vyakula vibichi. Kadiri miaka ilivyokwenda mbele watu waligundua moto kwa kupekecha vijiti. Ugunduzi huu uliwasaidia kuanza kuchoma nyama na kupika vyakula.



II Kadiri miaka ilivyosonga mbele ndivyo maendeleo yalivyopatikana. Badala ya watu kupata moto kwa kupekecha vijiti, waligundua pia njia nyingine. Njia inayotumiwa na watu wengi ni ile ya kutumia kibiriti. Kibiriti kikiwashwa tunaweza kupata moto wa kupikia kwa kuni, jiko la mafuta ya taa, jiko la makaa na jiko la gesi. Pia tunatumia kibiriti kwa kuwashia vibatari na kandili. Licha ya kupata moto wa kupikia na mwanga, kibiriti kinaweza kutupatia moto wa kuunguza mabiwi ili kuondoa uchafu katika mazingira tunamoishi.

III Moto pia unaweza kupatikana kwa njia ya umeme. Katika sehemu za miji watu wengi hupika kwa moto unaotokana na umeme. Pia hutumia taa za umeme ili kupata mwanga usiku. Wakati mwingine kama mtu akikosa kibiriti na hana njia nyingine ya kupata moto anaweza kutumia lensi. Lensi ikielekezwa kwenye mwanga wa jua kwa muda mrefu basi karatasi itakayowekwa chini ya lensi hiyo itashika moto.

IV Moto una faida nyingi sana kwa binadamu. Kwanza, unatupa mwanga wakati wa usiku. Katika miji yenye viwanda moto wa umeme ndio unaotumika katika kuendeshea mashine na mitambo mbalimbali. Kama moto usingegunduliwa, maisha ya watu yangekuwa duni.

V Moto ni mtumishi mzuri kama utatumiwa vema, lakini unaweza kuwa bwana mbaya kama ukitumiwa vibaya. Bila shaka umewahi kusikia ama kuona nyumba au kijiji kinaungua moto. Haya yanaweza kutokea tu tunapokosa kuwa waangalifu kwa matumizi ya moto.

VI Mara nyingi watu hutupa ovyo vipande vya sigara ama vijiti vya kibiriti vyenye moto. Vitu hivi vikitupwa mahali penye makaratasi, majani ama nyasi kavu moto unaweza kutokea na kuteketeza nyumba ama kijiji, na hata misitu. Ili kuepukana na hasara kama hizi rai hutolewa kwamba vipande vya sigara na vijiti visitupwe kabla ya kuvizima.

**KIFUNGU D**

# ■ *USMA yaiua Canon Yaounde 3-0*

**MOMBASA, Kenya**

❶ WAKATI Simba inaingia uwanja wa Taifa, Dar as Salaam kuivaa Ismailia ya Misri leo, washabiki wa timu hiyo ya Tanzania wanaoishi Mombasa wanatarajiwa kuwepo uwanjani.

❷ Gazeti la Coastweek la Mombasa, Kenya limeripoti kuwa wapenzi hao wa Simba kutoka huko wamejikusanya na kukodi basi ambalo litawafikisha Dar as Salaam kwa ajili ya kushuhudia mechi hiyo muhimu.

❸ Simba na Ismailia zitacheza katika mchezo wa Ligi ya mabingwa Afrika kuanzia saa 9 alasiri zikiwa na rekodi tofauti.

❹ "Wapenzi wa Simba wanajikusanya kwa ajili ya kukodi basi litakalowapeleka Dar es Salaam kuwahi mechi hiyo," linasema gazeti hilo.

❺ "Tunalazimika kwenda ili kuishangilia timu yetu ipate ushindi dhidi ya timu ya Kaskazini," alisema mshabiki mmoja ambaye aliipongeza Simba kwa kuifunga ASEC Mimosas ya lvroy Coast bao 1-0.

❻ Simba na Ismailia zilipambana mwaka juzi katika michuano ya Kombe la Washindi, lakini vijana wa Msimbazi wakajikuta wakitolewa na Wamisri hao.

❼ Ismailia iliifunga Simba rnabao 2-0 katika mchezo wa kwanza uliofanyika Misri, Simba ikashinda mabao kama hayo Dar es Salaam, lakini mchezo ukaahirishwa kutokana na mvua. Simba ilishinda bao 1-0 walipocheza tena na kutolewa.

❽ **Wakati huohuo**, katika mchezo wa kundi B, USMA ya Algena juzi iliibugiza Canon Yaounde mabao 3-0 katika mchezo uliofanyika mjini Algiers.

❾ Licha ya Canon Yaounde kuonekana kutawala mchezo huo ilijikuta ikilambwa mabao hayo ingawa wachezaji wake walilalamika kufungwa bao la tatu la penalti. Huo ni ushindi wa kwanza kwa timu hiyo ya Algeria.

❿ Katika hatua nyingine wapenzi wa soka wa Mombasa, wamewataka viongozi wa zamani wa timu ya Coast Stars FC kukutana na kujaribu kuirudisha timu hiyo katika medani ya soka ya kimataifa.

⓫ "Timu ilikuwa ikifanya vibaya katika hatua za mwisho, lazima kuna sababu," alisema mshabiki mmoja wa timu hiyo.

⓬ Shabiki huyo aliwaasa wadhamini wa timu hiyo, Mamlaka ya Bandari ya Kenya kuendelea kuidhamini timu hiyo, lakini kuwaachia viongozi wafanye shughuli zao za kiutawala na si maofisa wa mamlaka hiyo.

⓭ "Coast Stars ni timu ya watu wa Pwani ambao wanatakiwa kutoa kila aina ya msaada kwa ajili ya kuisaidia timu hiyo ili iendelee," alisema mshabiki mwingine.

⓮ Hivi karibuni, Coast Stars ilitolewa na timu ndogo, Taifa katika michuano ya Kombe la Rais.